



WIZARA YA NISHATI

JN HPP

MW 2115

Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia
Maji wa Julius Nyerere Hydro Power Project

Eneo: Pwani



KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA 2023/24

Kukamilisha ujenzi wa bwawa (main dam); ujenzi wa njia kuu za kupitisha maji (tunnels); ujenzi wa kituo cha kuongeza nguvu ya umeme (switch yard); na ujenzi wa nyumba za makazi na ofisi, kujenga njia ya kusafirisha umeme kutoka katika kituo cha kufua umeme (power house) hadi kituo cha kupokelea umeme (switchyard). Aidha, kazi zitakazoende-lea ni pamoja na ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme (power house); ufungaji wa mitambo ya kuzalisha umeme na ujenzi wa barabara za kudumu katika eneo la mradi.

Hadi kufikia mwezi Juni 2024, mradi wa kituo cha kuzalisha Umeme cha JNHPP utekelezaji wake umefikia asilimia 98.01. Mitambo mitatu kati ya tisa imewashwa ambapo kila mmoja una uwezo wa kuzalisha **235MW**.





UTEKELEZAJI WA MRADI HADI MWEZI JUNI 2024

Maendeleo ya Utekelezaji katika maeneo makuu ya Mradi hadi kufikia mwezi Juni 2024:-

- ▶ *Ujenzi wa bwawa (main dam) ni asilimia 99.42*
 - ▶ *Ujenzi wa Plunge pool ni asilimia 99.70*
 - ▶ *Ujenzi wa njia kuu za kuitisha maji (power waterways) ni asilimia 99.90*
 - ▶ *Ujenzi wa daraja la kudumu (permanent bridge) ni asilimia 97.21*
 - ▶ *Ujenzi wa kituo cha kuongeza nguvu ya umeme (switch yard) ni asilimia 99.96*
 - ▶ *Ujenzi wa nyumba za makazi na ofisi ni asilimia 98.55*
 - ▶ *Ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme (power house) ni asilimia 94.55*
 - ▶ *Ufungaji wa mitambo ya kuzalisha umeme (Installation works) ni asilimia 92.43*
 - ▶ *Ujenzi wa barabara za kudumu katika eneo la mradi ni asilimia 89.59*
- 